

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: +251 1 6634353
Nukushi: +251 1 627882
Simu ya Upepo: 21268 TANAD ET
Anuani pepe: addisababa@nje.go.tz
Tovuti: www.et.tzembassy.go.tz



Bole Kifle Katema 03/05
Kiwanja Na. 2213
S.L.P. 1077
Addis Ababa
ETHIOPIA

TAARIFA KWA UMMA

UMOJA WA AFRIKA NA TAASISI ZAKE WAANZA KUTUMIA KISWAHILI KAMA LUGHA YA KAZI YA UMOJA WA AFRIKA

Addis Ababa, 21 Aprili 2022

Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Umoja wa Afrika, Mhe. Balozi Innocent Shiyo, ameipongeza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kwa kuanza kutumia Lugha ya Kiswahili kama ya lugha ya kazi ikiwa ni utekelezaji wa Azimio la Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali la kutumia Kiswahili kama lugha ya Kazi ya Umoja huo lililotolewa mwezi Februari 2022.

Balozi Shiyo ametoa pongezi hizo leo tarehe 21 Aprili 2022, ikiwa ni kwa mara ya kwanza Mkutano wa 71 wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu ambao unafanyika mjini Banjul nchini Gambia kuanzia tarehe 21 Aprili 2022 hadi 13 Mei 2022 kutumia Kiswahili kama lugha ya kazi.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine utapokea na kujadili taarifa mbalimbali kuhusu hali ya haki za binadamu barani Afrika na kupokea taarifa kutoka kwa Nchi Wanachama, Tume za Haki za Binadamu na Asasi za Kiraia. Vilevile, pamoja na huduma za ukalimani, nyaraka mbalimbali za mkutano huo pia zitapatikana katika lugha ya Kiswahili.

Balozi Shiyo ameeleza kuwa, hatua hii ya kipekee inaifanya Lugha ya Kiswahili kuwa lugha pekee ya Kiafrika inayotumika kwenye Umoja huo na kwamba kutumika kwa lugha ya Kiswahili kutawezesha raia wa nchi za Afrika zaidi ya milioni moja kuweza kufuatilia shughuli za Umoja huo. Amefafanua kuwa, matumizi ya Lugha ya Kiswahili yatakuza zaidi mtangamano wa Afrika na kuchochea utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA) kama lugha ya biashara na ya mawasiliano mapana.

Pia ameongeza kusema kuwa, mbali na Mkutano huo, Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Taasisi zilizoko chini yake tayari zilianza kukitumia Kiswahili kama lugha ya kazi kwenye mikutano yake ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Pamoja wa Kamati ya Mabalozi/Wawakilishi wa Kudumu wa Nchi za Afrika kwenye Umoja wa Afrika na Mahakama ya Afrika uliofanyika Arusha, Tanzania mwezi Machi 2022. Kadhalika mwezi huohuo wa Machi 2022, Ubalozi wa Tanzania nchini Ethiopia ambao

unawakilisha pia Umoja wa Afrika, kwa mara ya kwanza tangu Umoja huu unuzishwe ulipokea Waraka wa Kibalozi ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili. Waraka huo ulikuwa unatoa mwaliko kwa Serikali ya Tanzania kushiriki katika Mkutano wa 14 Kamati Maalum ya Mawaziri wanaosimamia masuala ya Ulinzi, Amani na Usalama na Mkutano wa 17 wa Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

“Haya ni mafanikio makubwa sana katika kupigania matumizi ya Kiswahili kama moja ya lugha rasmi ndani ya Umoja wa Afrika. Nampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia suala hilo na ninatoa shukrani za dhati kwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kuratibu vema ushiriki wa Wakalimani wetu kwenye Mikutano,” amesisitiza Balozi Shiyo.

Itakumbukwa kuwa, katika Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari, 2022 Tanzania kwa mara nyingine tena ilifanikiwa kuingiza agenda ya Lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha ya kazi katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Katika Mkutano huu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwakilishwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alitoa hotuba yake kwa Kiswahili.

Miongoni mwa maeneo ya msisitizo yaliyoainishwa na Makamu wa Rais kuhusu agenda hiyo ni pamoja na; muda mwafaka kwa Umoja wa Afrika kuanza kutumia lugha asili za Afrika katika shughuli zake kwa kuanza na lugha adhimu ya Kiswahili ili kuwafikia na kuwatumikia watu wote Barani Afrika; matumizi ya Kiswahili yatatoa fursa kwa mamilioni ya waafrika ambao wanatumia Kiswahili kama lugha ya kwanza, lugha ya pili au lugha ya tatu kushiriki kikamilifu na kunufaika na fursa za Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA).

Wakuu wa Nchi na Serikali kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano huo wa 35 uliofanyika mwezi Februari 2022 waliielekeza Kamisheni ya Umoja wa Afrika kuweka mara moja utaratibu sahihi wa kuhakikisha Kiswahili kinaanza kutumika katika vikao vyote vya kisheria (statutory meetings) ifikapo Julai 2023.

IMETOLEWA NA:

UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI ETHIOPIA